
WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA DESEMBA 2024 - MACHI 2025





Imeandaliwa na;

**Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**

P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania
Phone: 0800114031 / 0800114032
E-mail: barua@wrbwb.go.tz
Website: www.wrbwb.go.tz

**Desemba, 2024**

## 1. UTANGULIZI

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kipindi cha Mwezi Desemba 2024 hadi Machi,2025 ili wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ujenzi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira waweze kuchukua tahadhari na hatua zaidi dhidi ya miundombinu pamoja na mali zao kutokana na ongezeko la maji linaloweza kujitokeza. Utabiri unaonyesha kupungua na kuongezeka kwa wingi wa maji katika vipindi tofauti tofauti ambapo Mwezi Desemba, 2024 tunategemea kuwa na ongezeko la wingi wa maji hadi kufikia mita za ujazo 253 kwa sekunde, kiasi hiki kitakuwa juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009 - 2023) katika Mwezi kama huo wa Desemba kutokana na Mvua za Vuli zinazotarajiwa kuendelea kunyesha hadi Mwishoni wa Mwezi Desemba, 2024[1]. Kipindi cha Mwezi Januari,2025 wingi wa Maji utapungua kidogo na kufikia wastani kutokana na kupungua kwa mvua katika *Catchment*, Aidha, Mwezi Machi, 2025 Wingi wa Maji unatarajiwa kuongezeka zaidi na kufikia hadi mita za ujazo 267 kwa sekunde ambapo itakuwa juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa mrefu kutokana na mvua za masika zinazotarajiwa kunyesha hali hii inaweza kupelekea uharibifu wa miundombinu pamoja na mali katika maeneo mbalimbali au kuchelewesha miradi ya ujenzi zinazoendelea kutekelezwa katika Wilaya za Mvomero, Morogoro, Kibaha na Bagamoyo, hivyo Bodi inazitaka Mamlaka husika kuchukua tahadhari stahiki ili kuzuia uharibifu unaoweza kujitokeza kutokana na ongezeko hilo la wingi wa maji.

### 1.1 ATHARI ZINAZOWEZA TOKEA

i. Uharibifu wa miundombinu na mali katika Mikoa ya Morogoro na Pwani
ii. Kuchelewesha utekelezaji wa miradi ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa mabwawa, Barabara, miradi ya maji katika Mikoa ya Morogoro na Pwani


.


[1] Taarifa ya Mwelekeo wa Mvua za vuli zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kipindi cha Mwezi Desemba,2024 hadi Machi, 2025 inaonyesha kiasi cha wingi wa Maji kitapungua na kuongezeka katika nyakati tofauti tofauti kutokana na mwelekeo wa Mvua za Vuli zinazoendelea kunyesha pamoja na mvua za masika zinazotarajiwa kunyesha (**Jendwali Na.1)**. Hatahivyo, Bodi inawaasa Mamlaka husika kuchukua hatua dhidi ya uharibifu wa mali pamoja na miundombinu utakaojitokeza kutokana na ongezeko la wingi wa maji katika Mto Ruvu

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu katika kituo cha *Ruvu river at* Morogoro road bridge (1H8A).**

| Jina la Mto | Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji | Kielelezo |
|---|---|---|
| *Ruvu river at Morogoro road bridge (1H8A)* | Utabiri unaonyesha Mwezi Desemba, 2024 na Machi, 2025 kutakuwa na ongezeko la wingi wa maji kati ya mita za ujazo 253 hadi 267 kwa sekunde, kiasi hiki kitakuwa juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009 - 2023) katika Miezi kama hiyo kutokana na Mvua za Vulin a masika zinazotarajiwa kuendelea kunyesha (**Kielelezo**). Aidha, Kipindi cha Mwezi Januari,2025 wingi wa Maji utapungua kidogo na kufikia wastani kutokana na kupungua kwa mvua katika *Catchment*, hali hii inaweza kupelekea uharibifu wa miundombinu pamoja na mali katika maeneo mbalimbali au |  |

<table>
<tr><td></td><td>kuchelewesha miradi ya ujenzi zinazoendelea kutekelezwa katika Wilaya za Mvomero, Morogoro, Kibaha na Bagamoyo</td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>Utabiri unaonyesha kwa Kipindi cha Mwezi Desemba 2024 hadi Machi 2025 wastani wa ujazo wa maji utafikia mita za ujazo milioni 1065 sawa na 59% ukilinganisha na wastani wa ujazo kwa Mwaka 2023/2024. Aidha,ujazo wa juu utakuwa mita za ujazo milioni 962.7 wakati ujazo wa kati utakuwa mita za ujazo milioni 255 na ujazo wa chini utakuwa mita za ujazo milioni 118.5.</td><td>
</td></tr>
</table>

## 3. USHAURI

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu inazishauri sekta za Kilimo, Madini, Utalii, Ufugaji na Uvuvi, Viwanda na usambazaji maji majumbani kuzingatia mambo yafuatayo; -

### a) Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini (UWSSA) na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA)

Bodi inazishauri Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuchukua tahadhari dhidi ya uharibifu wa miundombinu unaowezakujitokeza na kupelekea uhaba wa upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yao ya huduma kwa kipindi hiki cha kuongezeka kwa wingi wa maji kuanzia Mwezi Desemba,2024 hadi Machi, 2025.

### b) Kilimo

Bodi inashauri sekta kufanya mambo yafuatayo;-

i. Kuvuna maji ya mvua kwa kutumia mabwawa yaliyojengwa/yanayojengwa ili kuyahifadhi maji mengi kipindi hiki na kuyatumia kipindi cha kiangazi kwa ajili ya umwagiliaji

ii. Skimu zote za umwagiliaji kufunga mabanio za kuchepusha maji kutoka Mtoni katika kipindi hiki cha Mwezi Desemba,2024 hadi Machi, 2025 kutokana na mvua za vuli zinazoendelea kunyesha pamoja na mvua za masika zinazotarajiwa kunyesha ili kuepusha uharibifu wa miundombinu na mali zilizopo mashambani. Aidha, Wakulima wanashauriwa kutumia maji ya mvua katika kipindi hiki cha Mwezi Desemba,2024 hadi Machi, 2025 kukuza mazao yaliyopo mashambani au katika skimu zao za umwagiliaji.

iii. Skimu pamoja na wakulima wadogo wadogo kuondoa mazao yaliyokoma ili kuepuka uharibu wa mazao hayo katika kipindi cha Mwezi Desemba,2024 hadi Machi, 2025.

iv. Vilevile, Sekta iharakishe ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu zinazoendelea kujengwa.

### c) Ufugaji na Uvuvi

Bodi inashauri sekta kuchimba malambo ili kuhifadhi maji katika kipindi hiki cha maji mengi cha Mwezi Desemba, 2024 hadi Machi, 2025 ili yatumike kipindi cha kiangazi kunyweshea mifugo. Pia, wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa mifugo katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo katika mpango wa matumizi bora ya ardhi zilizopo katika Halmashauri za Wilaya.

Uvuvi wa kutumia sumu katika vyanzo vya maji hauruhusiwi.

**d) Madini**

Bodi inashauri Sekta ya Madini na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha uchimbaji na uchejuaji wa Madini unafanyika nje ya vyanzo vya maji ili kulinda ubora wa maji kwa watumiaji mbalimbali.

**e) Ujenzi**

Bodi inasisitiza sekta kuchukua tahadhari dhidi ya ongezeko la wingi wa maji kwa miradi inayoendelea kutekelezwa ikiwemo Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili kutokuathiri utekelezaji wa mradi Pamoja na usalama wa mradi kwa ujumla.

**f) Utalii**

Bodi inashauri wananchi na watalii kuchukua tahadhari ya usalama wao na mali zao dhidi ya Wanyama hatari waishio majini kwa kuwa katika kipindi cha Mwezi Desemba 2024 hadi Machi,2025 kina cha maji kitaongezeka Mtoni na kusababisha wanyama hao ikiwemo Mamba, Viboko, n.k kuhama kutoka katika kina kirefu na kukimblia katika maeneo yenye kina kifupi.

## 4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kufuatilia na kuwahabarisha Wadau wake juu ya utabiri huu wa mwenendo wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kutoa utabiri wa vipindi vifupi ili wadau waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya ongezeko au upungufu wa wingi wa maji utakaoweza kujitokeza.